

HOTUBA YA IJUMAA.

Kuutumia wakati na hatari za kuupoteza

Imefasiriwa na

Profesa.Ayman Alasar

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mwenyezi Kusema ndani ya Kitabu chake Kitukufu:

وَالْعَصْرِ * إِنَّ الْإِنْسَانَ لَفِي خُسْرٍ * إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ وَتَوَاصَوْا بِالصَّبَرِ.

{Naapa kwa Zama * Hakika binadamu bila ya shaka yumo katika hasara * Ila wale walio amini, na wakatenda mema, na wakausiana kwa haki, na wakausiana kusubiri}. Ninashuhudia kuwa hakuna Mola wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na Mtume wake, ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma amani na baraka kwake Mtume pamoja na Maswahaba zake na watu wa nyumbani kwake na wale woe waliomfuata kwa wema mpaka siku ya kiyama.

Baada ya utangulizi:

Wakati una umuhimu mkubwa na thamani kubwa katika uhai wa mwanadamu, nao ni kwa ajili ya neema ambayo ameineemesha Mola Mtukufu kwetu, ambapo anasema Mola wa haki:

وَسَخَّرَ لَكُمُ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ دَائِبِينِ وَسَخَّرَ لَكُمُ اللَّيلَ وَالنَّهَارَ * وَآتَاكُمْ مِنْ كُلِّ مَا سَأَلْتُمُوهُ وَإِنْ تَعْدُوا
نِعْمَةَ اللَّهِ لَا تُحْصُوهَا.

{Na akalifanya jua na mwezi kwa manufaa yenu endelevu, na akaufanya usiku na mchana kwa manufaa yenu * Na akakupeni kila mlichohu muomba. Na mkihesabu neema za Mwenyezi Mungu hamuwezi kuzidhibiti}.

Mwenye kuzingatia ndani ya Quran Tukufu atakuta kuwa imechunga wakati kwa uzito mkubwa, ambapo kuna Sura nne ndani ya Quran zimeitwa kwa jina la baadhi ya nyakati, nazo ni “Suratul-Fajri, Suratul-Layli, Suratul-Dhuhaa na Suratul-Asri”,

kama vile Mwenyezi Mungu Mtukufu ameapa kwa nyakati sehemu nyingi, ambapo anasema Mola Mtukufu:

وَالْفَجْرِ * وَلَيَالٍ عَشْرِ * وَالشَّفْعِ وَالْوَتْرِ

{Naapa kwa alfajiri * Na kwa masiku kumi * Na kwa viwili viwili na kimoja kimoja}.

Na anasema tena Mola Mtukufu:

وَالصُّحَى * وَاللَّيلِ إِذَا سَجَى

{Naapa kwa mchana * Na kwa usiku unapo tanda!}. Na anasema tena Mola Mtukufu:

وَالصُّبْحِ إِذَا أَسْفَرَ

{Na kwa asubuhi inapo pambazuka}. Na anasema Mola Mtukufu:

وَاللَّيلِ إِذَا يَعْشَى * وَالنَّهَارِ إِذَا تَجَلَّى.

{Naapa kwa usiku unapo funika * Na mchana unapo dhihiri}.

Umuhimu mkubwa unaotolewa na Quran kwenye wakati inatuonesha uzito uliopewa na wajibu wa kuutumiwa vyema katika matendo ya heri ambayo yananufaisha nafsi jamii na nchi, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

فَاسْتِبْقُوا الْخَيْرَاتِ

{Basi shindanieni mema}. Na anasema Mtume SAW:

اغتنِمْ خمْسًا قَبْلِ خَمْسٍ: شَبَابَكَ قَبْلَ هَرَمِكَ، وَصِحَّتَكَ قَبْلَ سَقَمِكَ، وَغَنَاكَ قَبْلَ فَقْرِكَ،
وَفِرَاغَكَ قَبْلَ شُغْلِكَ، وَحِيَاكَ قَبْلَ مُوتِكَ

"Tumia vizuri mambo matano kabla ya matano: Ujana wake kabla ya uzee wako, afya yake kabla ya kuumwa kwako, utafiri wako kabla ya umasikini wako, nafasi yake kabla ya kushuhurishwa kwako na uhai wako kabla ya kifo chako". Na anasema Hassan Al-Hassan Al-Basary R.A: Ewe binadamu hakika wewe ni masiku, kila inapoondoka siku imeondoka sehemu yako.

Hivyo ni lazima kwetu kupangilia wakati wetu na kunufaika na kila sehemu ya wakati, na kufanya kazi ya kutumia vyema kila sehemu ya wakati wa maisha yetu, kwani harakati huzaa harakati na uvivu huzaa uvivu, na kidogo kwenye kidogo ni kingi, na maisha ya

mwanadamu ni ibara ya mkusanyiko wa nyakati ambazo kwa ujumla wake na muundo wake hutengeneza maisha yake yote. Msemaji anasema:

Mapigo ya moyo ya mtu ni yenyeye kumwambia – hakika uhai ni ibara ya dakika na sekunde.

Tunasisitiza kuwa umri wa mwanadamu na uhai wake wa kweli ni kile anachozalisha katika urithi wa kimaarifa, au kifikra, au uzalishaji wa elimu ya kinadharia au vitendo, na kila anachokifanya kwa ajili ya huduma ya wanadamu, pasi ya kuangalia kiwango cha muda ambao anaishi, anasema mshairi:

Umri wa kijana na utajo wake na wala si urefu wa muda wake – na kifo chake kudhalilika kwake na wala si siku yake.

Hivyo fufua utajo wako kwa wema – utakusanya kwa hilo uhai wa aina mbili.

Baraka katika umri haiwi kwa kuishi umri mrefu tu bali ni kiwango anachozalisha au kukitoa mwanadamu katika huu umri kwa ajili ya kuhudumia dini yake au dunia yake au dunia ya watu, mtu bora ni mwenye umri mrefu na matendo mazuri, na mtu muovu ni mwenye umri mrefu na kuwa na matendo maovu, na mtu bora ni mwenye manufaa zaidi kwa watu, kwani Mtume SAW aliulizwa: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni nani mtu bora? Akasema SAW: “Mwenye umri mrefu na matendo mazuri” aliulizwa ni yupi mtu muovu? Akasema: Mwenye umri mrefu na matendo maovu” na anasema Mtume wetu SAW: Mtu anayependwa zaidi na Mwenyezi Mungu ni mwenye manufaa zaidi kwa watu”

HOTUBA YA PILI:

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimwendee mbora wa viumbe naye ni Mtume wetu Muhammad SAW pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Kama vile Sharia ya Kiislamu imetuhimiza juu ya umuhimu wa kutumia vizuri nyakati, kwani imetutahadharisha na kitendo cha kujisahau pamoja na hatari za kuupoteza wakati, ambapo anasema Mola Mtukufu:

وَأَنْفَقُوا مِنْ مَا رَزَقْنَاكُمْ مِّنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ فَيَقُولَ رَبِّ لَوْلَا أَخْرَجْنِي إِلَى أَجَلٍ قَرِيبٍ
فَأَصَدَّقَ وَأَكُنْ مِّنَ الصَّالِحِينَ * وَلَنْ يُؤَخِّرَ اللَّهُ نَفْسًا إِذَا جَاءَ أَجَلُهَا وَاللَّهُ خَيْرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ.

{Na toeni katika tulicho kupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Hunicheleweshei muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema? * Wala Mwenyezi Mungu hataichelewesha nafsi yeyote unapo fika muda wake; na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayo yatenda}

Na anasema Mtume SAW:

نِعْمَتَانِ مَعْبُونُ فِيهِمَا كَثِيرٌ مِّنَ النَّاسِ الصَّحَّةُ وَالْفَرَاغُ

“Neema mbili zimepunjwa ndani yake kwa watu wengi nazo ni, afya na muda”.

Na anasema tena Mtume SAW:

لَا تَرُوْلُ قَدْمًا عَبْدٍ يَوْمَ الْقِيَامَةِ حَتَّىٰ يُسْأَلَ عَنْ أَرْبَعٍ خِصَالٍ: عَنْ عُمُرٍهِ فِيمَا أَفْنَاهُ؟ وَعَنْ شَبَابِهِ فِيمَا أَبْلَاهُ؟
وَعَنْ مَالِهِ مِنْ أَيْنَ اكْتَسَبَهُ وَفِيمَا أَنْفَقَهُ؟ وَعَنْ عِلْمِهِ مَاذَا عَمِلَ فِيهِ؟.

“Hauondoki mguu wa mja siku ya kiyama mpaka aulizwe mambo manne: Kuhusu umri wake ameumalizia kwenye nini, kuhusu ujana waka ameumalizia kwenye nini, kuhusu mali zake amezipata wapi na amezitumia vipi, na kuhusu elimu yake ameifanyia kazi ipi”.

Na anasema tena Mtume SAW:

تَصَدَّقُوا قَبْلَ أَنْ لَا تَصَدَّقُوا

“Toeni sadaka kabla ya kufungwa muda wa kutoa sadaka”.

Kuna baadhi ya watu ni wenye kuiba wakati, ikiwa hawataiba wakati wanajaribu kuuwa wakati, kwa sababu yupo na muda, akiwa hayupo kwenye amri ya dini yake wala amri ya dunia yake, ambapo anasema Abdillah Ibn Mas'oud RA: Hakika mimi nachukia kumuona mtu anapoteza muda, akiwa hayupo kwenye kazi za kidunia wala kwenye matendo ya akhera.

Ni kwa kiasi gani tunahitaji kujenga nyakati zetu kwa yale yenye manufaa kwetu, na kunufaika jamii yetu na nchi yetu ili kufikia mafanikio maendeleo furaha duniani akhera.

Ewe Mwenyezi Mungu turuzuku baraka katika nyakati zetu na umri wetu.